

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI
JESHI LA POLISI TANZANIA

Anuani ya Simu "MKUUPOLISI"
Simu: (026) 2323585
Fax Na: (026) 2323586



Ofisi ya Mkuu wa Jeshi la Polisi,
Makao Makuu ya Polisi,
4 Mtaa wa Posta,
S.L.P 961,
40483 DODOMA.

31/01/2022

TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

Ndugu waandishi wa habari,

Kumekuwepo taarifa nyingi za kudhania na upotoshaji kuhusiana na tukio la kujinyonga hadi kufa kwa Mkaguzi Msaidizi wa Jeshi la Polisi Grayson Mahembe huko Mkoani Mtwara. Jeshi la Polisi Tanzania lingependa kutoa ufafanuzi wa tukio hilo ili kuondoa upotoshaji wa makusudi na mijadala inayoendelea.

Ndugu waandishi wa habari,

Mkaguzi Msaidizi huyu aligundulika kujinyonga tarehe 22.1.2022 akiwa mahabusu kutokana na tuhuma za kukiuka sheria za nchi za kumnyang'anya fedha na kisha kumuua kijana aliyefahamika kwa jina la Mussa Hamis na kisha kuutupa mwili wake vichakani huko katika kijiji cha Namgogori mkoani Mtwara tarehe 5.1.2022.

Baada ya kufanya tukio hilo la ukiukwaji wa viapo vyao akiwa na wenzake, wakiwepo Maafisa, Wakaguzi na Askari wengine, hawakutoa taarifa kwa viongozi wao kwa sababu walifahamu kuwa wamefanya hivyo kwa nia ovu, kwa tamaa zao na kinyume cha sheria za nchi.

Baada ya taarifa za tukio hilo kuwafikia viongozi wa Polisi Mkoa wa Mtwara, walianza uchunguzi ikiwa ni pamoja na kuwakamata askari waliokuwa wanatuhumiwa.

Ndugu waandishi wa habari,

Miongoni mwa askari waliokamatwa na kuanza kuhojiwa ni huyo Mkaguzi Msaidizi wa Polisi Grayson Mahembe. Alipohojiwa alieleza mtiririko mzima wa matendo waliyofanya na mwisho akawapeleka Maafisa waliokuwa wanafanya uchunguzi wa tukio hili sehemu

walipoutupa mwili wa Mussa Hamisi na maelezo yake yaliandikwa na yakawa yamelandana na ushahidi mwingine uliokuwa umeshakusanywa (maelezo hayo yapo).

Baada ya hatua hiyo aliwekwa katika mahabusu ya peke yake na ndivyo pia ilifanyika kwa wale askari wengine kwani hata baadhi yao ilibidi wapelekwe mahabusu za Mkoa wa Lindi ili wasiharibu ushahidi uliokuwa unaendelea kukusanywa.

Ndugu waandishi wa habari,

Baadaye ndipo ikagundulika Greyson Mahembe amejinyonga. Baada ya tukio hilo taratibu zote za ukaguzi wa matukio zilifuatwa ikiwepo kupiga picha na zipo kwa kutumia wataalam wa kuchunguza matukio kama hayo. Picha hizo zinaonesha dalili zote za mtu aliyejinyonga. Mwili ulifanyiwa uchunguzi pia (postmortem) na daktari wa kuweza kuthibitisha kama kifo kilitokana na kujinyonga au ni sababu zingine. (taarifa za uchunguzi huo zipo).

Ndugu waandishi wa habari,

Kuna maneno pia kutoka kwa baadhi ya watu wakiwepo ambao tumeona labda wamesahau taratibu za mazishi ya askari aliyejinyonga au aliyejitoa uhai wake kuwa Mkaguzi Msaidizi huyu hakuzikwa kijeshi.

Jeshi la Polisi lingependa kutoa ufafanuzi kuwa, askari yeyote anayefariki katika hali ya kujitoka uhai, hazikwi kijeshi, kwa maana kwamba hakuna gwaride la mazishi litakalochezwa na risasi au mabomu ya kishindo kupigwa, kwani anahesabiwa kama hajafa kishujaa na hastahili heshima hiyo. Taratibu nyingine hufanyika kama kumpeleka katika eneo atakalozikwa kulingana na matakwa ya familia na ndivyo ilivyofanyika.

Aksanteni kwa kunisikiliza

Imetolewa na:

David A. Misime - SACP

Msemaji wa Jeshi la Polisi

Makao Makuu ya Polisi

Dodoma, Tanzania

www.polisi.go.tz

www.twitter.com/tanpol

www.facebook.com/tanpol

www.instagram.com/polisi.tanzania